MILAMBO CO-OPERATIVE UNION LIMITED
P.O.BOX 186 HEAD OFFICE - URAMBO
REG NO. AFF-TBR-URA-DC-2023-57
WE STRENGTHEN OUR ECONOMY

# MBINU BORA ZA USIMAMIZI WA UZALISHAJI WA TUMBAKU KWA WAKULIMA



## 1. KABLA YA MSIMU (JULAI – AGOSTI)

- Saini mkataba na **AMCOS/** mnunuzi.
- kuchagua aina ya mbegu iliyopendekezwa (mfano: K326, Kilimo K).
- kupima udongo (lengo la pH: 5.5–6.5).
- Chagua shamba lenye historia nzuri ya mzunguko wa mazao (miaka 3–4 bila kupanda mazao ya jamii ya tumbaku).
- Andaa na rekebisha  mabani ya kukaushia pamoja na mifumo ya mabomba ya joto.
- Nunua mbegu, mbolea na viuatilifu.
- Panga bajeti ya msimu na mahitaji ya nguvu kazi.




## 2. KUANDAA KITALU (AGOSTI – OKTOBA)

- Andaa kitalu kwa ajili ya kusia mbegu kwa kuzingatia vipimo vilivyo pendekezwa kitaalamu ( urefu m30 kwa upana m1).
- Sia mbegu mwezi Agosti au Septemba.
- Mwagilia miche mara kwa mara kwa kutumia maji safi.
- Weka mbolea kwenye kitalu kulingana na maelekezo ya kitaalamu ( N P K 10:18:24 kilo 5/ kitalu).
- Linda miche dhidi ya wadudu na magonjwa kwa kufanya ukaguzi angalau mara moja kwa wiki.
- Izoeshe miche hali ya hewa ya shambani kwa siku 7–10 kabla ya kuipandikiza shambani.



## 3. MAANDALIZI YA SHAMBA (SEPTEMBA – NOVEMBA)

- Ondoa visiki, magugu na mabaki ya mazao yaliyopita.
- Weka chokaa au samadi kulingana na matokeo ya upimaji wa udongo.
- Tengeneza matuta kwa kufuata mwinuko wa ardhi ili kuzuia mmomonyoko wa udongo kwa kuzingatia vipimo vya kitaalamu ( nafasi kati ya tuta na tuta ni m 1.1 – 1.2 m).
- Tayarisha kinga moto (firebreaks) kuzunguka mashamba na mabani).



## 4. UPANDIKIZAJI SHAMBANI (NOVEMBA – DESEMBA)

- Pandikiza miche baada ya mvua ya kwanza yenye kiwango cha angalau milimita 25.
- Chagua miche yenye afya na inayolingana urefu na unene ( urefu wa sm 20 na unene wa penseli).
- Mwagilia miche kwa mbolea ya maji mara tu baada ya kupandikiza.
- Weka nafasi ya m1.1–1.2  kati ya mistari/tuta na m 0.5–0.6  kati ya mimea.
- Badilisha miche iliyokufa au iliyoathirika ndani ya siku 5–7 baada ya upandikizaji.



# 5. UTUNZAJI WA SHAMBA (NOVEMBA – FEBRUARI)

- Weka mbolea kwa mgao wa mara 3–4 kwa kiwango kilichopendekezwa kulingana na afya ya udongo au hali ya hewa.
- Hakikisha shamba halina magugu, hasa katika wiki 6 za mwanzo.
- Fanya ukaguzi wa shamba kila wiki  hili kudhibiti wadudu (mfano: vidukari na viwavi) na magonjwa (Kwa kutumia viuwatilifu vilivyoendekezwa kitaalamu).
- Katia maua kabla hayajachanua katika hatua ya ukuaji wa mche ili kupata majani 16–20 kwa kila mmea. ( inategemea aina ya mbegu, udongo na hali ya hewa).
- Dhibiti machipukizi (suckers) mara moja kwa njia ya mikono au kwa kutumia viuatilifu. (Yamaotea).







## 6. UVUNAJI NA UKAUSHAJI (JANUARI – APRILI)

- Vuna majani yakiwa yamekomaa, kutoka kijani-kibichi kuelekea njano.
- Chuma majani 2–3 kutoka kila mmea kila baada ya siku 5–7.(inategemea aina ya mbegu na hali ya hewa).
- Hifadhi majani kwenye sehemu safi na yenye kivuli wakati wa kuvuna.
- Suka majani kwenye mianzi kwa kuzingatia nafisi iliyopendekezwa kitaalamu.
- Panga mianzi kwenye bani kwa nafasi ya kutosha ili kuruhusu mzunguko wa hewa.
- Pakia mianzi kulingana na uwezo wa bani.
- Fuata hatua za ukaushaji (kufanya jani kuwa njano → kuimalisha rangi ya jani → kukausha jani → kukausha migongo ya jani).
- Dhibiti joto na unyevunyevu mara kwa mara.
- Tumia nishati salama na zingatia usalama wa moto.



## 7. UCHAMBUZI NA MASOKO (FEBRUARI – JULAI)

- Hakikisha majani yana kiwango cha unyevu unyevu unaoruhusiwa kitaalamu.
- Chagua eneo la kuchambulia na kuhifadhia tumbaku kwa kufuata maelekezo ya kitaalamu.
- Fuata misingi ya uchambuzi wa tumaku kitaalamu (mpamgilio wa jani kwenye shina, ubora, rangi, hitilafu , ufupi na urefu wa jani).
- Ondoa vitu vyote visivyo tumbaku (NTRM).
- Funga na weka alama kwa kufuata masharti ya mnunuzi.



## 8.BAADA YA MSIMU (MEI – JUNI)

- Ondoa na haribu mabaki (mabua) yote ya mazao ili kuzuia kuenea kwa wadudu na magonjwa msimu unaofuata.
- Safisha na karabati mabani, stoo na vifaa vyote.
- Fanya tathmini ya mavuno, ubora, na changamoto kwa maandalizi bora ya msimu ujao





Imeandaliwa na

**IDARA YA UZALISHAJI**
**CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA**
**MILAMBO**